SEHEMU YA KUMI NA SITA

M ENGINEYO

Mahudhurio ya Wabunge Bungeni

117. Kuhudhuria vikao vya Bunge ni wajibu wa kwanza wa kila Mbunge. Mbunge yeyote atakayeshindwa kuhudhuria Mikutano ya Bunge mitatu mfululizo, bila ruhusa ya Spika iliyotolewa kwa maandishi atapoteza Ubunge wake.

Taarifa Rasmi

118.-(1) Shughuli za Bunge zitaendeshwa katika lugha ya Kiswahili au ya Kiingereza, bila tafsiri ya lugha hizo kutolewa.

(2) Taarifa Rasmi ya Majadiliano Bungeni, ikiwa katika lugha iliyotumiwa na msemaji, na pia ikiwa karibu kabisa ya neno kwa neno, itatayarishwa chini ya usimamizi wa Katibu kwa kufuata maagizo yatakayotolewa na Spika kwa ajili hiyo.

(3) Kila Mbunge aliyetoa hotuba Bungeni atapewa nakala ya hotuba yake mapema iwezekanavyo, ili aweze kusahihisha makosa ya uchapaji, kama yatakuwapo. Lakini Mbunge hataruhusiwa kubadilisha maana halisi ya maneno aliyoyasema Bungeni.

Mavazi Rasmi

119.-(1) Bila ya kuathiri masharti yanayofuata ya Kanuni hii, kila Mbunge anayeingia katika Ukumbi wa Bunge atawajibika kuvaa mavazi

ambayo ni safi na yenye kuhifadhi heshima yake yeye, hadhi ya Bunge na utamaduni wa nchi, kama ilivyoainishwa katika fasili ya (3) ya Kanuni hii.

Vazi Rasmi la Spika

(2) Vazi Rasmi la Spika litakuwa ni joho lenye kuonyesha rangi za bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa na baadhi ya mazao makuu nchini, lililoshonwa maalum kwa ajili hiyo, ambalo litavaliwa juu ya vazi lolote ambalo ni vazi rasmi kwa Wabunge kwa mujibu wa fasili ya (1) ya Kanuni hii.

(3) Vazi rasmi kwa Wabunge litakuwa lolote kati ya haya yafuatayo yaani:-

(a) Kwa Wabunge Wanawake:-

(i) Vazi lolote la heshima yaani ambalo si la kubana mwilini, na ni refu kukiuka magoti;

(ii) Kanga au kitenge kinachovaliwa pamoja na blauzi ya rangi yoyote;

(iii) Suti ya kiulaya ya kike, ama ikiwa kamilifu pamoja na kofia na *"gloves"* au bila vitu hivyo.

(b) Kwa Wabunge Wanaume:

(i) Suti ya Kitanzania ya mikono mirefu au mifupi, ambapo koti lake lina *"collar"*;

(ii) Suti ya Kitanzania ya mikono mirefu au mifupi, ambapo koti lake lina shingo ya mviringo;

(iii) Shati la Kitanzania lenye shingo ya mviringo la mikono mirefu au mifupi la rangi moja tu, pamoja na suruali ya rangi yoyote;

(iv) Vazi la Kimwambao, yaani kanzu, koti na kofia;

(v) Suti kamili ya kiulaya ya rangi yoyote;

(vi) Koti aina ya *"blazer"* na tai, pamoja na suruali yoyote ya heshima.

(4) Vazi rasmi la Katibu na Wasaidizi wake Bungeni litakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kwa Makatibu Wanaume:-

Ama suti kamili ya Kitanzania yenye shingo ya mviringo yenye mikono mirefu na rangi nyeusi au bluu, au suti kamili ya Kiulaya ya rangi nyeusi au bluu, na shati jeupe na tai.

(b) Kwa Makatibu Wanawake:-

Suti ya Kiulaya ya Kike, kama ilivyoelezwa kwa Wabunge Wanawake, lakini ikiwa ya rangi nyeusi au ya bluu.

(5) Mpambe wa Bunge na Wasaidizi wake ndani ya Ukumbi wa Bunge watavaa mavazi rasmi ambayo yataamuliwa na Spika mara kwa mara.

(6) Isipokuwa kwa idhini maalum ya Spika, kandambili, viatu vya michezo au viatu vinginevyo visivyokuwa rasmi havitavaliwa Bungeni.

(7) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya (6), Spika anaweza, kwa sababu maalum, kumruhusu Mbunge au mtu mwingine anayehusika na shughuli Bungeni kuvaa viatu ambavyo siyo rasmi.

Bendera ya Bunge

120. Kutakuwa na Bendera rasmi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo itaitwa Bendera ya Bunge na itakayokuwa katika sura na rangi kama ifuatavyo:-

Itakuwa na rangi ya bluu iliyoiva, iliyo katika umbo la msitatiri, ikiwa na umbo dogo la Bendera ya Taifa ndani yake katika pembe ya juu upande wa kushoto.

Itakuwa pia na Siwa ya Bunge yenye rangi ya dhahabu, na chini kukiwa na Utepe wenye maneno **"Bunge la Tanzania."**

Matumizi na Upepezaji wa Bendera ya Bunge

121.-(1) Bendera ya Bunge itapepezwa katika maeneo yafuatayo:-

(a) Katika Ofisi za Bunge Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar.

(b) Nje ya Ofisi za Wabunge zilizopo Makao Makuu ya Mkoa, Wilaya na katika Majimbo ya Uchaguzi.

(c) Ndani ya Ofisi ya Mbunge katika meza anayofanyia kazi.

(d) Katika magari binafsi ya Wabunge ambapo Bendera hiyo itapepezwa ikiwa mbele upande wa kushoto wa gari la Mbunge wakati Mbunge mwenyewe anapokuwa ndani ya gari hilo, na akiwa anaendeshwa na dereva mwingine, siyo anapokuwa anaendesha mwenyewe.

Isipokuwa kwamba Mbunge hatapepeza Bendera kwenye gari lake awapo katika Miji ya Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar, na anapokuwa anatumia gari la kukodi au la kuazima.

(2) Spika na Mawaziri ambao ni viongozi wenye stahili ya kupepeza Bendera za Serikali katika magari yao waweza kupepeza kwenye magari yao ama Bendera ya Serikali au Bendera ya Bunge kama watakavyoona inafaa (lakini siyo zote mbili kwa pamoja).

(3) Bila kuathiri masharti yaliyotangulia ya Kanuni hii, Bendera ya Bunge itapepezwa kuanzia saa 12.00 asubuhi na kuteremshwa mara ifikapo saa 12.00 jioni kila siku.

Isipokuwa kwamba Bendera itaendelea kupepezwa katika gari la Mbunge baada ya saa 12.00 jioni endapo Mbunge huyo atakuwa safarini hadi pale atakapomaliza safari yake.

Matumizi yasiyo-ruhusiwa ya Bendera ya Bunge

122. (1) Bila ya kujali masharti ya sheria nyingine za nchi, ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia Bendera ya Bunge kwa matumizi yafuatayo:-

(a) Kama vazi la kuvaa mwilini au kufungwa katika sehemu yoyote ya mwili, au shuka ya kujifunika.

(b) Kwa namna yeyote ile yenye lengo la kibiashara.

(c) Kwa namna nyingine inayoashiria kulidhalilisha Bunge.

(2) Mbunge yeyote hataruhusiwa kupepeza Bendera ya Bunge iliyochakaa, ama kwa kuchanika, au kwa kuchuja.

(3) Ni marufuku kwa mtu au kampuni yoyote kubuni na kutengeneza Bendera inayofanana na Bendera ya Bunge kwa matumizi yoyote.

Kukashifu Bendera ya Bunge

123. Mbunge au mtu mwingine yeyote ambaye:-

(a) atafanya kitendo chochote, atatoa matamshi kwa mdomo au kwa maandishi au kuchapisha maneno yoyote kwa lengo la kukashifu au kuifanya Bendera ya Bunge idharauliwe,

(b) atakiuka masharti ya Kanuni za matumizi ya Bendera ya Bunge,

atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria ya *Parliamentary Immunities Powers and Privileges Act, 1988 (No. 3 of 1988)* ana atastahili adhabu chini ya Sheria hiyo.

Kutengua Kanuni za Bunge

124. - (1) Kwa idhini ya Spika, yoyote kati ya Kanuni hizi yaweza kutenguliwa kwa madhumuni mahsusi baada ya Waziri kutoa hoja kwa ajili hiyo.

(2) Hoja inayotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii haitahitaji kutolewa taarifa, na itaamuliwa bila mabadiliko wala mjadala wowote.

(3) Maelezo ya hoja ya kutaka kutengua Kanuni yoyote itakuwa ni pamoja na maelezo kuhusu madhumuni ya kutaka kanuni hiyo itenguliwe.

(4) Kanuni inayotenguliwa itatenguliwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa tu, na siyo kwa madhumuni mengine yoyote.

Kufanya Mabadiliko katika Kanuni

125. -(1) Bunge laweza wakati wowote, kwa kupitisha Azimio kufanya mabadiliko katika Kanuni yoyote kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Kanuni za Bunge. Mabadiliko yaliyopitishwa yataanza kutumika mara moja.

(2) Endapo Kanuni za Bunge zitafanyiwa mabadiliko, Spika aweza kuagiza Kanuni hizo zichapishwe upya kwa madhumuni ya kuingiza mabadiliko yote yaliyofanywa.

(3) Nakala za Kanuni zilizochapishwa kwa kufuata utaratibu huu zitahesabiwa kuwa nakala halisi za Kanuni za Bunge zilizofanyiwa mabadiliko.

Mambo yasiyo-wekewa masharti

126. Iwapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti katika Kanuni hizi; Spika ataamua desturi na utaratibu wa kufuatwa katika jambo au shughuli hiyo na uamuzi huo pia utaingizwa katika Kitabu cha Maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadaye.

Kanuni kuanza kutumika

127. -(1) Kanuni hizi zitaanza kutumika katika Mkutano wa Bunge uliozipitisha, mara baada ya kupitishwa hivyo.

Kufuta Kanuni za Mwaka 1987

(2) Kanuni za Bunge la Tanzania za mwaka 1987 zinafutwa na hazitatumika tena katika kuendesha shughuli za Bunge.